KUELEKEA TEOLOGIA YA WOKOVU YA KISALVATORIANI

Padri Thomas Perrin SDS

1 Januari 2015[1]

UTANGULIZI

Mtakatifu Agostino aliwahi kuandika "Ee Mungu unawaamsha wanadamu kufurahi katika kukusifu, kwa sababu umetuumba kwa ajili yako mwenyewe, na mioyo yetu kamwe haitatulia hadi itakapotilia kwako." Sentensi hii ina teologia nzito inayohusika moja kwa moja na kwa ujumla swala la wokovu. Kwa upana wake, kile alichoumba Mungu kikiwa tengefu naye, yaani mbali na Mungu mwenyewe, kadiri ya mpango na utashi wa Mungu, kimepangiwa kurudi kwa Mungu na kupumzika katika Mungu. Hivyo wokovu unaweza kuwa:

1) 1. Mchakato ambao, kwao, mpango wa Mungu unatimilizwa "....kama mpango kwa utiimilifu wa nyakati, wa kutimiliza vitu vyote katika Kristo huko mbinguni na duniani." (Ef. 1, 10). Au
2) Kama tunda la mwisho la huo mchakato, yaani, uzima wa milele katika Mungu.

Yesu Mwokozi wetu, na roho mtakatifu wamefunua mpango wa Mungu wa wokovu na kupitia mpango huo, kwa namna kubwa sana kazi ya wokovu ilianza katika historia ya mwanadamu. Nafsi hizo mbili za Mungu zinapotuingiza katika njia hiyo ya wokovu , sisi binadamu tukiwa na uelewa wa Mungu pamoja na kazi yake kwetu sisi na ndani yetu, sisi sote tumeitwa sio tuunde "utumwa au kifungo cha kijamii, kiutamaduni au kiufundi". Ila tumeitwa kufanikisha muungano wetu na kristo .(***mwanga wa mataifa 1***). Hapo, tukiwa tumemezwa na upendo wa Mungu, kila chozi litafutwa (Is. 25,8) na tutamtukuza Mungu daima (Uf 5:13) Mungu atakayekua yote katika yote (1 Kor. 15;28).

KUELEKEA TEOLOGIA YA WOKOVU YA WASALVATORIANI.

Sasa, wasalvatoriani wanafuata njia gani kuelekea teologia ya wokovu? Ngoja tuainishe vifungu muhimu. Kwanza, kuwa mfuasi wa yesu duniani, tunatakiwa kuzama kwa undani katika mahusiano ya upendo na Mungu wetu, sisi wenyewe, ili tuweze kuwaongoza wengine. Tusije tukawa viongozi vipofu wanaojaribu kuwaongoza vipofu wengine. Mahusiano haya ya ndani na Mungu yanafahamika kwa wasalvatoriani kama "kumjua Mungu". Kisha Mungu anatuita kushirikiana naye pamoja na wenzetu na wengine katika kazi ya wokovu. Tunatafuta, siyo wokovu wetu tu, bali pia wa watu wengine.

Pamoja na Maria, mama yake, tunawapelekea wengine Mwokozi, ambaye tumemfahamu sisi wenyewe (Hati ya Familia ya Kisalvatoriani # 10)

Kamwe hatutapumzika hata kwa dakika moja iwapo kuna mwanadamu mmoja ambaye hamjui na kumpenda Mungu katika vitu vyote. (chapter , prefel line 1). Kumfahamu an kumpenda Mungu ndiyo maneno muhumu katika teologia yetu ya wokovu. Sisi sote

[1] Please note: the endnotes for the Kiswahili translation of this article were not translated.

tumeitwa kuwa wajumbe wa matumaini kwa watu wanaohitaji mwelekeo, wanaohitaji kutiwa nguvu, wanaohitaji upendo wa ndani na wenye mahusiano ya upendo na Mungu mwokozi wao. Tunatakiwa "kuwaongoza wengine kuelekea kwenye haki,"tufahamu ya kuwa kinachofanya watu kuwa na maumivu ni nguvu ambazo mara nyingi ziko nje ya uwezo wao. Pengine ni kwa sababu ya dhambi au ujinga wa weingine, ambao husababisha maumivu katika maisha yao.

"***Pamoka na Maria, mamake, tunakuwa wajumbe kwa wengine kwa kumchukua mwokozi ambaye tumemfahamu kwa wwengine." (HATI #10)***

Tunatafuta kuwaongoza wengine kwenye uhuru, iwe minyororo yao ni ya kiroho, kimwili, kiakili, kivionjo, ya kifamilia, au kijamii. Tunamsaidia Mungu kuwafungua kutoka utumwa wao kwa dhambi, iwe kimwili au kiroho, iwe utumwa wa muda mrefu, au ulioanza karibuni tu, ni sehemu ya wito wetu.Mwishowe tumeitwa kuwasaidia watu kila mahali wamjue Mungu, wampende Mungu, wamtumikie na kufikia muungano wa milele na Mungu, ni kazi ya maisha yetu. Mabadiriko ya kijamii pia, ni kazi ya maisha yetu: wote watawatimikia wengine kama ndugu katika Mwokozi.

KUMJUA MUNGU

Hamna teologia ya wokovu ya wasalivatoriani inaweza kukamilika bila kutilia maanani maneno au msemo huu " Kumjua Mungu." Mtu akipitia kwa haraka Mwongozo wa maisha, Katiba na Sheria za jumla za Masista wa Mungu Mwokozi, vyote vinaeleza matumaini ya kuwa wote wamjue Mungu na Yesu Kristo aliyemtuma, na meneno haya yemetumika mara nne. Haya ni marudio ya kiuaminifu ya (yoh: 17.3) " ***NA UZIMA WA MILELE NDIO HUU WAKUJUE WEWE, MUNGU WA PEKEE NA WA KWELI NA YESU KRISTO ULIYEMTUMA"***. Pia Katiba inaeleza nia ya kumfanya Mungu, au Yesu, au "Yeye" ajulikane, mara tisa zaidi. Haya yote yanatuonesha msisitizo mkubwa kwenye sehemu hii ya karisma yetu sisi wasalivatoriani . Tuangalie mifano michache:,

Katiba namba 4. Inatafakarisha: " Yesu kama Mwokozi wa dunia ni kiini na chanzo cha maisha yetu. kutoka kwake tunajifunza kuwa na kiu ya utukufu wa Mungu, kama waanzilishi wetu walivyfanya. Hamu yetu ya kuwa wake kabisa, na kushiriki katika kazi yake ya wokovu, inatuvuta kumjua kwa karibu zaidi na kumutumikia bila kujibakiza." Kiteolojia, Mungu, anayetupenda kwanza, ndiye anayetupa zawadi ya kumpenda! Mungu hutuvuta katika umungu wake, kwa ukaribu zaidi, kwa kutualika tumjue, na hivyo kumpenda na kumtumikia. Kadiri tunavyozidi kumpemjua Mungu kwa karibu zaidi, ndivyo tunavyoweza kumpenda zaidi. Tunavyompenda zaidi Mungu, ndivyo tunavyotafuta kufanya mapenzi yake, kwa kumtumikia yeye na wengine kwa moyo wote, tukitii amri za Mungu, tukimsifu na kumtukuza Mungu, nk.

Katiba namba 20, inaanza na kumjua Mungu na kuchukua elimu maarifa na upendo wa Mungu kwenye hatua nyingine. Tunafanya kila jitihada kuwa na utafiti wa ndani kwa roho ya Mungu. Tumewekwa wazi kwa upendo wake Mungu na tunaendelea kuweka uhuru, kuwapenda wote kama kristo alivyotupenda. Uwepo wake kwetu unatufanya tuwe na amani an furaha na inatufanya sisi kuendelea kueneza uzuri wake na upendo wake wa wokovu kwa

kila mtu tutakayekutana naye katika maisha yetu. Hapa tunafahamu ya kuwa "kumjua mungu"aitajwi lakini matunda ya elimu ni "roho ya bwana inafanya kazi kwa kila mtu na inatuzaidia kuwa wawazi na uhuru kuelekea upedo wa mungu".Mtu anaweza kusema ya kuwa katiba ya shirika inamfanya Mungu ajulikane. "fadhili na kweli zimekutana, haki na amani nimebusiana (zab 85)"

Injili ya mtakatifu yohane sura ya kumi, ni ya manufaa zaidi hapa. Hapa mwandishi anatumia maneno yenye maana zaidi katika injili hii ya mtakatifu Yohane, mwinjili anatumia vitenzi "kumjua" na wasomi wengine wanasadiki kuwa vitenzi hivi vinabadilika badilika. Yoh 17;3 inaonyesha kitenzi "ginoskein" ambao ni kitenzi hiki "kumjua mungu" inaonyesha kufahamu mtu mwingine viziri kuliko kitenzi, yaani kuwa na ufahamu katika haya ya injili ya yohane ndio tunapata "*ginoskein*" imetumika sana. "mimi ndimi mchungaji mwema, nao walio wangu nawajua nao walio wangu wanijua mimi , kama vile baba anijuavyo, nami nimjuavyo baba ....."Yoh 10;14-15. Hapa ni matumizi mara nne ya nomino *ginoskein* kwa sentensi moja, lakini kiteologia inahusiana sisi binadamu kwa kumjua Mungu. Hapa kuna uiwano kati ya ufahamu wa binadamu na wa Mungu pia.

Zaidi ya hayo, mchungaji kuwajua kondoo wake kunahitimishwa na yeye hutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo zake.(Yoh 10;11), hivyo kujua na kupenda ni kitu kimoja. Na kuwajua kondoo zake ni muhimu, mchungaji anajua kondoo zake kwa majina, huwaita kondoo wake kwa majina yao na kondoo pia wanamfuta.(Yoh 10: 3-4). Kama mwokozi wetu anajua kondoo zake na anawapenda kuwalinda hadi kufikia katika kifo chake kwa kuwaita majina nao kwa kusikia sauti ya mchungaji wao na kumfuata. Hii ni aina moja ya upendo wa kipekee au wa ndani na ni funzo tumejifunza kutoka kwa mwandishi Yohane.

MAISHA KATIKA UKAMILIFU WAKE.

Hati ya familia ya kisalvatorian inatukumbusha wito wetu, tufanye kazi ili watu wote, popote pale waweze kuwa na mang'amuzi ya maisha kamili kwa kupitia kristo mwokozi wetu. ***(hati ya Mtaguso wa Vaticano 1 namba1).*** Tunapotetea hii, tunaweka karisimu yetu ili iweze kueleweka kwa ajili ya wokovu. Tunapowakaribisha wengine katika utimilifu wa maisha, tunakuwa wakala kwa niaba ya Mungu. {**U-kimataifa wetu...kuendeleza Kazi ya Yesu ya kutoa uhai ya kuleta wokovu kwa viumbe vyote, na ukombozi kutoka kila kilicho tishio kwa ukamilifu wa uhai}.** Tunakua vyombo vya Mungu katika mipango yake ya wokovu, wakati huo huo, wakati wa ukamilifu wa maisha ni uzima wa milele ndio kitu Mungu amatuita kwa kila mtu. Na pia sisi sote tumeitwa kuwaleta au kuwasaidia binadamu na viumbe vyote kwa Yesu kristo ambaye ndiye uzima wa milele. Tunapojitoa maisha yetu kwa ajili hiyo, tunajibu wito wetu kwa Mungu kwa kuendelea kumsaidia katika kazi yake ya wokovu. Hapo hapo tuna wajibu kwa kila binadamu kumjua Mungu ipasavyo na kumpenda kikamilifu na pia kwa kujitoa bila kujibakiza kwa Mungu. Hii itakuja kutambulikana au kueleweka mbinguni wakati kama ilivyoelezwa hapo juu. ***" MUNGU AWE YOTE KATIKA YOTE***" (1 kor 15:28).

Kama alivyosema Mtakatifu Agostino tutapata pumziko la kweli na la milele katika uwepo wa Mungu ambaye ni kila kitu. Itaeleweka ya kuwa, umungu wa Mungu ndiyo ukamilifu wa wokovu wetu. Tutaishi kwa ajili ya Mungu, kuishi ndani ya Mungu na mwishowe kulisifu

jina la Mungu milele na milele. Katika injili ya Mtakatifu Yohane, ambapo Yesu na Baba (MUNGU) ni wamoja, Yesu kristo mwokozi wetu, atakuwa na mwisho wa njia ya wokovu. Alisema "nami nikiinuiwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu"(YOH 12;32). Sisi tulikombolewa, tutaunganishwa katika mwili wa fumbo wa Kristo (1Kor. 12: 12-27), na pamoja tutatengeneza uwepo, ambao ni Kristo aliyefikia ukamilifu wake (Eph 4: 13).

KUSOMA ALAMA ZA NDANI ZA NYAKATI

Sisi wasalivatoriani tumeitwa au kualikwa "tusome daima alama za nyakati" (rej. ***Gaudium et sp namba 4***) na tutende kadri ya alama za nyakati ili utume wetu eweze kuzaa matunda mema na mengi.Habari nyingi na mambo mengi ya ulimwengu yanajazana ili yapate kusikilizwa nasi. Tunaweza kujimaliza wenyewe katika kusikiliza habari hizo, ili kutafuta alama za nyakati. Ingawa kusikiliza alama za nyakati ni muhimu, wakati mwingine muhimu zaidi ni kusikiliza alama za nyakati zilizo mioyoni na akilini mwa watu. Hebu tufikirie jambo hili, baadhi ya watu wanasema nasadiki kwa Mungu au nasadiki kwa Yesu, lakini ni nadra sana mtu huyu kusali au pia kufika Kanisani kwa ajili ya Misa Takatifu**.** Upendo wao wa Ekaristi uko wapi? Upendo wao kwa Neno linalorutubisha na kutoa maisha? Upendo wao kwa Kanisa Katoliki, uko wapi? Baadhi ya watu wanakuwa na wasiswasi ya kuwa uenda wataenda jehanamu, na matumaini yao ya ndani ni kwamba watakwepa hukumu na kwenda mbinguni. Wanateseka kwa kutokuwa na mahusiano mema na Mungu ambaye ni mwenye haki , na mwenye huruma anayejua kila kitu na pia mwenye upendo wa dhati kwa wote. Wakristo wengine wanakuwa na mashaka juu ya uwepo wa jehanamu, na wana imani ya kuwa Mungu mwenye upendo atawaonea uruma na kuwakaribisha kwenye uzima wa milele bila mchakato wowote wa hukumu. Bado wengine wanaungama dini yao kwa woga, na wanasali kwa uangalifu, bila kufahamu kwa uhakika namna ya kumkumbatia Mungu kama rafiki yao.

"Roho yetu ya u-kimataifa... tunajiweka wazi kwa maswali na changamoto za nyakati zetu za kihistoria, tukiruhusu ishara za nyakati kufunua kwetu namna na njia ya kuitikia." (Hati ya Familia ya kisalvatoriani # 8a.

Kama mitazamo hii ndio iko katika mioyo na akili za waumini, wawe wenye bidii, au wavivu, je kwa wale ambao sio waumini ni nini kinakuwa ndani ya mioyo yao na akili zao? Wengine wanamsadiki Allah na kwa mtume Mohamed, lakini wanaheshimu kristo kwa umbali sana, kama wanamfikiria hata kidogo.

Wengine wanasadiki mafundisho ya Buddha, na wengine wanamheshimu na kumtukuza Budhha. Ndugu zetu wayahudi wanaamini na kukubali maadndiko ya kiberania, lakini sio maandiko ya wakristo. Orodha ya imani nyinginezo ambazosiyo za kikristo ni ndefu na imani hizo zipo nyingi ulimwenguni. Sasa tunaweza kuwaendeaje kuwapelekea habari njema ya Bwana wetu Yesu Kristo? Ni jinsi gani tutaweza kuwapa ujumbe wa wokovu wa Yesu msulibiwa? Hizi ni baadhi ya Alama za nyakati na zinagusa karisima yetu. Kila binadamu, awe Mkirsto, aliyewahi kuwa Mkristo, au asiye Mkristo kabisa, wote tunahitaji kuwa wasikivu. Kisiri siri hao wengine wanaweza kuwa wanatuuliza, wokovu ni nini? Na pia, mimi nitaokolewa? Au wanaweza wasituulize hayo maswali, kwa sababu ya kutokujua kwao,

wanaweza wasiwe na wazo lolote juu ya Mungu, Muumba wetu mwenye upendo, kwa Yesu Mwokozi wetu, au kwa Roho Mtakatifu

Padri Francis Maria wa Msalaba Jordan na mama Maria wa mitume, walitilia maanani sana kile kinachoendelea ndani ya mioyo na akili za watu. Kama mfuasi wa Yesu , na kwa kujisikia kuitwa na Mungu kuanzisha shirika ambao litashirikiana na Mungu katika kuokoa roho za watu, padri Jordan alianzisha kundi la watu, walei wa kiume an wa kike , na masisita, mabruder na mapadre ili wafanye kazi pamoja kama kundi na waende duniani kote kama wafuasi, kuwafundisha watu wote kumfahamu na kumpenda Mungu na Yesu kristo mwana wa Mungu na mwokozi wetu. Wafuasi hawa wangegundua waliopo waumini hao na wangefanya kazi kwa umakini zaidi, kwa kuwatia watu moyo, kwa moyo chanya, na wakati mwingine hata kwa utani, na kuwaongoza katika nia ya haki na kusahihisha makosa yaliyo ndani ya watu, kwa kuyabadirisha kwa ukweli wa Mungu. Mungu atawaongoza kama watakuwa wazi kwa neno la Mungu, kwa uwazi na ufahamu mpya wa Mungu, maisha baada ya kifo, mbingu, jehanam, Mpango wa Mungu, Msamaha wa Mungu, Kanisa la Kristo, Sakramenti kama msaada wa Mungu unaotolewa kwetu kutokana na Upendo wake, nk.

Tunafuata mfano na uongozi wa kuvutia wa padri Jordan na wa Maria wa mitume ili tumtangaze kwamba, pamoja na mashaka yanayoweza kutuvuta kufikiri vinginevyo, Yesu Kristo ni kweli " njia na ukweli, na uzima, mtu haji kwa baba, ila kwa njia ya (Yesu)" (Yoh 14;6). Hata ingawa kuna mkanganyiko na woga kuhusu Yesu, kuwa na uhakika wa maisha ya milele, Yesu mwenyewe ndio njia, ukweli na chanzo cha uhai na uzima wenyewe wa kimungu.

WOKOVU:KUWAONGOZA WENGINE KATIKA UHURU, MAHALI PA WAZI.

Kuna namna nyingine ya wokovu, yaani kuwaongoza watu wengine kuelekea katika njia ya uhuru katika uwazi. Wakati njia hii ilikua si wazi sana miaka ya sabini, bado ina maana siku hizi. Namna hiyo inazingatia kazi ya Mungu ya wokovu kwa wayahudi waliokua utumwani kule misri. Maisha yao yalikuwa ya dhiki na ya maumivu sana. " wakafanya maisha yao kuwa uchungu kwa kazi ngumu, kazi ya chokaa na matofali, na kazi ya mashamba kazi zao zote walizowatumikisha kwa ukali" (kutoka 1;14) kutoka kwa mateso au matatizo yao, Mungu aliwaokoa aliwatoa katika utumwa wao kule misri wakiongozwa na mtumishi wake Musa.

Sisi wasalvatoriani pia tumeitwa kuwasaidia watu na kuwaongoza kutoka katika shida na vifungo vyao, kutoka katika pingu na minyororo yao. Tunatakiwa kuwaponya kutoka woga wao wa ndani na kutoka maumivu yao ya nje. Tunatakiwa kuponya majeraha yao, tuwape mahitaji yao ya kila siku na ya kiafya ili wawe na nguvu. Pia tunatakiwa kuwafuta machozi yao na ikifaa tuwape furaha. Tunamuomaba mwokozi wetu atusaidie ili tuweze kuwaongoza watu hadi wafike katika nchi ya ahadi yenye amani ,furaha, na matumaini. Na hayo ndiyo maisha aliyotuahidi Bwana wetu Yesu Kristo.

YESU KRISTO ALPHA NA OMEGA.

Yesu kristo ni uzima wenyewe .....na ni ukamlifu wa uzima. Kama sisi wasalvatoriani tunaweza kuwa na teologia yoyote ya wokovu, lazima ikamilike katika wazo hili. Mwokozi anayeongoza njia zetu, mtoto anayejua hali yetu ya kibinadamu (kimwili) kijana msomi na ambaye anauliza maswali, mwinjili, rafiki na mwalimu, mponyaji, anayewalisha wenye njaa, rafikki wa watu wa mataifa, wenye dhambi, wanawake, watoto, waliokataliwa, wanyonge, fukara, wanaoteseka na wakimbizi; Bwana wa mitume, Mwana wa Maria..... mwenyewe ni maisha ya kimungu. Yote tunayoweza kusema kuhusu wokovu yataishia/ yatakamilika ndani yake (Kristo). Yeye ndiye Alpha na Omega, wa kwanza na wa mwisho (rej. Ufunuo 1;8) Kristo uzima wetu njoo utuokoe.

Reflection Questions[2]

1 Soma tena hati ya familia ya kisalvatoriani kwa haya maswali ya kutafakali
   a) Andika au eleza maneno au sentensi inayokugusa na ujiulize: " Sentensi hii inaniambia nini, na ni jinsi gani naweza kuitikia?
   b) Familia ya kisalvatoriani inaweza kuwa na maana gani katika eneo lako la Dunia, na kwa ulimwengu mzima?
2. Baada ya kusoma makala haya, ungepewa nafasi ya kufanya marudio ya Hati ya Familia ya Kisalvatoriani, ungeongeza au kubadirisha nini?
3. "To work with God for the Salvation of souls" (Fr. Jordan). What does this mean today for me/us? How would I translate it into today's language?

[2] Please note: the reflection questions for the Kiswahili translation of this article were not translationed.